

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAAA
HALMASHAURI YA WILAYA MOSHI
MTIHANI WA PAMOJA WA MUHULA WA KWANZA
MSIMBO:021 KISWAHILI KIDATO CHA TATU
MUDA: SAA 3 MEI 2026

MAELEKEZO:

1. Mtihani huu una sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali 11
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na B kila sehemu ina maswali 10
la tisa (9) ni la lazima
3. Sehemu A ina alama 16, B alama 54
4. Zingatia maelekezo ya **kila sehemu** na jumla ya alama
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi
6. **Hautakiwi** na **hauruhusiwi** kuingia na vitu vyovyote visivyoruhusiwa katika chumba cha mtihani
7. Kumbuka kuandika namba yako katika **kila ukurasa wa karatasi** utakazojibia

SEHEMU A (ALAMA 16)

- 1) Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo
 - i. “shangazi yupo shambani kwake”kifungu hiki cha maneno kipo katika ngeli gani?
 - A. I-ZI
 - B. YU-A-WA
 - C. PA-MU-KU
 - D. KI-VI
 - E. U-I
 - ii. Obogo alifurahi **alipopata** maswali yote ya kiswahili.neno lililopigiwa mstari ni
 - A. Nomino
 - B. Kielezi
 - C. Kitenzi
 - D. Kishazi tegemezi kielezi
 - E. Kishazi tegemezi kivumishi
 - iii. Mtazamo unaoeleza kuwa kiswahili kilianzia lamu ilitolewa na nani
 - A. Mazrui na sharif 1994
 - B. Masamba 2002;2007,2017
 - C. Archipelago,nurse na spear,1985
 - D. James der ver allen 1993
 - E. Chiraghdin 1971;1973&1974
 - iv. Ifuatayo ni moja ya sifa ya mhakiki wa kazi ya fasihi
 - A. Awe anamfahamu mwandishi kwa undani
 - B. Awe amesoma kazi nyingi za fasihi
 - C. Hapaswi kumpa mwandishi ari ya kuendelea na uandishi
 - D. Awew zao la jamii inayoandikiwa
 - E. Awew ameandika kazi moja tu
 - v. Upi ni uchanganuzi sahihiwa mofu zinazounda kitenzi **watachekeshana?**
 - A. Wa-ta-che-ke-sha-na
 - B. Wata-cheke-sh-ana
 - C. Wa-ta-chek-esh-a-na
 - D. Wa-ta-ch-ek-e-esh-an-a

- E. Wa-ta-chek-esh-an-a
- vi. Mifano ya maneno yaliyoundwa kwa njia uambatanishaji ni
- Shughulisha,polepole,mtutu
 - Pigapiga,pigilia,mapigo
 - Baruapepe, isimujamii, pakashume
 - Mwimbishaji,banguabongo,chajio
 - Hatimiliki,utaifishaji,vilevile
- vii. Ipi ni sababu muhimu ya kutumia lugha kulingana na muktadha
- Kuzuka kwa matukio mbalimbali
 - Kuendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia
 - Kumudu shughulininayofanyika
 - Kupamba mazungumzo
 - Kuwezesha mawasiliano
- viii. Ipi kati ya zifuatazo ni sahihi katika kanuni za uandishi wa dayalojia?
- Ubanaji wa maneno maelekezo ya vitendo na anwani za wahusika
 - Maelekezo ya vitendo matumizi ya vihisishi na anwani ya wahusika
 - Matumizi ya vihisishi,maelekezo ya vitendo na uzingatia wa muwala
 - Uzingatiaji wa mantiki, ujenzi mzuriwa uhusika na saini za wahusika
 - Uzingatiaji wa muwala anwani za wahusika na ubanaji wa maneno
- ix. Neno **shurutishwa** limeundwa na silabi ngapi?
- Tano
 - Nne
 - Tatu
 - Sita
 - kumi
- x. Ipi ni tofauti ya msingi kati ya mashairi ya ngonjera
- Mpangilio wa vina na mizani
 - Idadi ya mizani na mishororo
 - Majibizano baina ya watu wawili au zaidi
 - Mpangilio maalumu wa silabi na lugha ya mkato
 - Mapigo ya kimuziki na ridhimu

2) Oanisha maswali ya sehemu A na majibu yake katika sehemu B

SEHEMU A	SEHEMU B
A. Mambo ambayo msanii wa kazi ya fasihi inawasilisha katika jamii yake	A. Fasihi
B. Watu au wanyama anaowatumia mwandishi kubeba ujumbe fulani katika kazi ya fasihi	B. Maudhui
C. Hali ya pande mbili kukinzana katika maswala ya kijamii	C. Riwaya
D. Kazi ya sanaa inayotumia lugha ya mazungumzo au maandishi kufikisha ujumbe kwa hadhira	D. Mhakiki
E. Tamathali ya semi ambayo vitu au viumbe wasio binadamu hupewa nafasi ya kutenda kama binadamu	E. Tashihisi
F. Mtu anayechambua kazi ya fasihi kwa weledi	F. Fani
	G. Wahusika
	H. migogoro

SEHEMU B (ALAMA 54)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

- 3) i) Matumizi ya kiimbo hubainisha lengo la mzungumzaji. Fafanua malengo ya mzungumzaji katika sentensi zifuatazo,
- a) Mwanafunzi anasoma kwa bidii
 - b) Mwanafunzi, soma kwa bidii
 - c) Mwanafunzi anasoma kwa bidii?
 - d) Mwanafunzi anasoma kwa bidii!

ii) Eleza mofimu iliyobebwa na kila mofu iliyopigiwa mstari. Toa mofimu moja kwa kila mofu

- a) Kijitabu hiki hakisomeki vizuri
- b) Amekwenda sokoni kununua mchele na maharage
- c) Jitu lile linapenda kuabudiwa
- d) Akifika mwambie aje ofisini kwangu
- e) Anapenda kusoma mashairi kkutoka kitabuni

- 4) i) Kwa kutumia mfano mmoja kwa kila hoja bainisha taarifa tatu za kisarufi zilizopo katika vitenzi vya kiswahili

ii) Tunga sentensi moja kwa kutumia maneno yafuatayo

- a) “vizuri” litumike kama kiwakilishi
 - b) “Wale” litumike kama kitenzi kikuu
 - c) “Alikuwa” litumike kama kitenzi kishirikishi
- 5) i) Uanishaji wa ngeli za nomino kwa kigezo ha upatanisho wa kisarufi hutegemea vitu vitatu vitaje

ii) Kwa kila nomino ifuatayo bainisha viambishi vya o rejeshi vya umoja na wingi katika ngeli

- a) Magari
- b) Kijana
- c) Upepo
- d) Kabati
- e) Chumba
- f) miti

- 6) i) Kwa kutoa mifano fafanua dhana ya tungo

ii) Tunga hufanya kazi mbalimbali katika lugha ya kiswahili. oneshwa ukweli wa kauli hii kwa kufafanua kwa ufupi kazi tano za tungo. Toa mfano ka kila kazi

- 7) Ukuaji na ueneaji wa kiswahili umepitia vipindi vingi tofauti tofauti, fafanua kwa mifano mambo manne yaliyosaidia kukuza na kueneza lugha ya kiswahili kipindi cha wajerumani
- 8) Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata

Lugha yoyote hasa lugha inayokua na iliyo hai inatokana na mazingira ya watu na utamaduni wao. Kiswahili ni lugha ya Afrika mashariki iliyoenea na kujulikana na wengi zaidi katika Afrika mashariki kuliko lugha nyingine yoyote ya Afrika. Umaarufu umeifanya ikubalike kuzungumzwa ndani ya bunge la Afrika mashariki na katika vikao vya kimataifa.

Ajabu ni kwamba watu ambao wanadai eti Kiswahili ni lugha ya kigeni, yaani asili yake si Afrika. Tena bila aibu wanadiriki kuwataja waarabu kuwa waasisi wa lugha hiyo adhimu ya Kiswahili eti kwa sababu tu yapo baadhi ya maneno ya Kiarabu yaliyoingizwa ktika msamiati wa Kiswahili kama vile elimu, enzi, laki, thumuni, sultani, kauli, hadhi na kitabu.

Wapo baadhi ya wengine wanaoshikilia kuwa utamaduni wa Kiswahili ni wa kigeni, lakini Kiswahili hakina wenyewe kwa vile hakuna kamwe watu hao waitwao waswahili. Kiswahili

kumetokana na muunganiko wa lugha zaidi ya moja kama vile ilivyo **thubutu** kuwa ya afrika na utamaduni wake una **ithibati** kamili kuwa ni utamaduni wa Afrika.

Dhana yenye mashiko kwa baadhi ya wasomi ni kwamba utamaduni wa kiswahili chimbuko lake ni mwambao wa Afrika mashariki. Ukichukua tawi lolote la mila na desturi za kiswahili kuwa shina lake la Afrika, maneno kama vile harusi,ada,malezi,itikadi yoyote yana **shadidia** hilo.

MASWALI

- a) Andika kichwa kinachofaa kwa habari hii.
- b) Taja mawazo makuu mawili yanayojitokeza katika habari hii
- c) Kutokana na habari uliyosoma wasomi wana msimamo gani kuhusu lugha ya Kiswahili?
- d) Toa maana ya maneno yakliyopigiwa mstari katika habari hii

SEHEMU C (ALAMA 30)

Jibu maswali mawili tu kutoka katika sehemu hii,swali la tisa(9) ni la lazima.

- 9) Mhakiki hufanya kazi ya uhakiki katika kazi za fasihi, fafania sifa za mhakiki bora.
- 10) Fasihi simulizi inaweza kuhufadhiwa kwa njia tofauti tofauti.fafania ubora na udhaifu wa kuhifadhi fasihi simulizi kwenye maandishi.
- 11) Usanaa wa fasihi hujitokeza katika vipengele mbalimbali muhimu. Onesha usanaa hu